Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 1 Issue 1 | [November] [2024] | [Page 93] – [Page 105]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

# Uvulivuli wa Tafsriri kutoka Lugha za Asili kwenda Lugha ya Kiswahili Mfano wa Albamu ya Kikinga ya Sumasesu Theatre Art Group

**Arnold B. G. Msigwa**[1]
[1] Taasisi ya Taaluma za LughaChuo Kikuu cha Kabale
agawasike@gmail.com

**Article History:**
**Received:** 27 Aug 2024
**Accepted:** 21 Oct 2024
**Published:** 11 Nov 2024

**Maneno muhimu: Uvulivuli katika Tafsriri; Lugha za Asili; Kiswahili**

*This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license*
cc BY NC ND

## Ikisiri

Katika taaluma ya tafsiri, uvulivuli wa matini zilizotafsiriwa umejikita zaidi kwenye tafsiri za lughaza kigeni kwenda lugha za asili au lugha za asili kwenda lugha za kigeni. Mathalani tafsiri ya Kiingereza kwenda Kiswahili ama Kiswahili kwenda Kiingereza (Maro, 2018). Chukulia[94] ikiwa ni kwamba uvulivuli huo unatokana na wafasiri kutokuwa na umilisi wa lugha za kigeni hasa Kiingereza, na ama tofauti za kiutamaduni baina ya lugha mbili; yaani matini chanzi na matini lengwa. Jitihada kidogo zimejishughulisha na uvulivuli wa tafsiri zilizotafsiriwa kutoka lugha za asili kwenda Kiswahili na athari zake kimawasiliano. Utafiti huu ulichunguza Uvulivuli wa Tafsiri kutoka lugha ya Kikinga kwenda lugha ya Kiswahili mfano Albamu ya Sumasesu Theatre Art Group. Sampuli ya utafiti huu ni nyimbo tano za Albamu ya Sumasesu Theatre Art Group. Usampulishaji tabakishi ndiyo ulitumika kupata nyimbo hizo. Data zilikusanywa kwa njia ya uchanganuzi matini, ambapo nyimbo zilisikilizwa mara tatu, kisha kudondoa tafsiri iliyotolewa kutoka lugha ya Kikinga kwenda Kiswahili zenye uvulivuli kwa kuzingatia kaida za lugha ya Kikinga. Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima (Nida, 1964) na kuendelezwa na Nida & Tiber, (1969). Data zilichanganuliwa kwa njia ya maudhui na kuwasilishwa kwa njia ya majedwali na ufafanuzu kutolewa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa kuna utumiaji wa visawe vya lugha ya Kiswahili ambavyo si sahihi katika tafsiriiliyotolewa kiasi cha kuhamisha maana ya msingi ya matini chanzi. Mathalani, maana ya msingi ikibatilishwa, ujumbe uliolengwa katika matini chanzi unaathiriwa na hivyo kumfanya msikilizajiwa matini lengwa kutopata athari iliyolengwa na msanii. Kutokana na uvulivuli huo, makala yanapendekeza utafiti mwingine na mpana zaidi kufanyika kuhusu tafsiri za kutoka lugha za asili kwenda lugha ya Kiswahili kutumia data pana zaidi. Utafiti kama huo ukifanyika unaweza kubadilimtazamo wa wana nadharia kwamba, uvulivuli wa tafsiri ni tokeo la wafasiri kutojua lugha wanazozishughulikia au tofauti za kiisimu kati ya lugha chanzi na lugha lengwa; kwa sababu kiisimu Kikinga na Kiswahili zote ni lugha za Kibantu na pia waliofasiri nyimbo hizo ni wazawa waKikinga na ambao sio wazawa wa Kiswahili.

# Translation Opacity of Native Language Texts into Kiswahili: Example of song in Sumasesu Theatre Art Group Album


## Abstract

In translation, the opacity of translated text is mainly focusing on translations from foreignlanguages to native languages, such as English – Kiswahili or Kiswahili – English (Maro, 2018). The reason for focusing on that type of translated text assumes that this opacity is caused by inabilityof English language of many translators, that is, the incompetence in linguistic and cultural norms of target language. Little has been made in assessing the opacities of translated text from native language into Kiswahili language and their communication implications. This research describes theopacity of translation text from Kikinga to Kiswahili. Five selected Kikinga songs from Sumasesu Theatre Art Group were analyzed. The selection was stratified sampling. Text analysis was used asa method for data collection. The selected songs were listened to three times. The content and formanalysis were applied to make judgment on the text that has semantic and form opacities with regardto Kikinga language. The research was guided by Nida (1964) Translation Theory of "Functional Equivalence" as extended by Nida and Tiber, (1969). The findings are presented using tables and descriptions. The results show that Kiswahili equivalents and synonyms which have been used to transfer the message from Kikinga language are not correct to the extent that they have different meaning in regard to source text as intended by song writer. The reason for the errors are not well known, but it seems the translator has low knowledge of both Kikinga and Kiswahili language. When the basic meaning of source text has been altered in target text, then it affects the intended massage to the audience. Due to these opacities, the article suggests further wider research to assessthe opacity of translation from native language to Kiswahili. This type of research if undertaken, canchange the perspective that the opacity of translated text from foreign language to native (Kiswahili)is due to language inability of translators, linguistic and cultural variation.

**Key words: The Translation Opacity, Native Language Texts, Kiswahili**

## 1.0 Utangulizi

Cartford (1995) anasema kutafsiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja na kuweka, badala yake, mawazo yanayolingana nayo kutoka lugha nyingine. Fasili hii ina maanisha kuwa kinachofasiriwa katika matini ni ujumbe au maana na siyo miundo ya lugha husika.Kwa upande mwingine Mwansoko na wenzake (2015) wanafafanua tafsiri kuwa zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Ufafanuzi wa dhana yatafsiri kwa mujibu wa Cartford (1995) na Mwansoko na wenzake (2015) zinadhihirisha mwoano. Kulingana na ufafanuzi wao, tafsiri inaweza kufafanuliwa kuwa kuhamisha mawazo au ujumbe ulio katika maandishi kutoka katika lugha moja kwenda katika lugha nyingine. Hata hivyo, kuna kuhawilisha mawazo yaliyo katika mazungumzo na kuweka katika maandishi kama wafanyavyo wanaofasili nyimbo.

Mtunzi au msanii wa wimbo huweza kuzungumza na kuruhusu ufasiri wa maneno yaliyoandikwa kupeperusha chini ya runinga kwa ajili ya hadhira kutambua maana na ujumbe wa wimbo au mazungumzo. Aidha, wakati mwingine mtunzi au msanii wa wimbo huweza kuzungumza kwenye runinga huku fasiri ya mazungumzo yake yakitolewa chini yake kwa ajili ya hadhira pana. Utafiti huu ulihusu kuchunguza tafsiri iliyofanyika kwenye matini zinazozungumzwa (imbwa) na kupitisha

ujumbe wa kimaandishi wa tafsiri chini uso wa runinga.

## 2.0 **Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Tafiti nyingi zinazohusu uvulivuli wa tafsiri zimeelekea kujishughulisha na tafsiri kutoka ama lugha ya kigeni kwenda Kiswahili ama kutoka lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha za kigeni hasa Kiingereza. Mwelekeo huu unaelekea kuwa umesababishwa na wafasiri wa awali ambao walimakinikia kazi zilizoandikwa kwa lugha ama ya Kiingereza na kuzitafsiri kwa kuzipeleka katika Kiswahili. Baadhi ya kazi zilizohawilishwa kutoka Kiingereza kwenda katika Kiswahili ni pamoja na tafsiri ya Oedipus the King – Mfalme Edipode iliyofasiriwa na Samwel S. Mushi (1962), Merchants of Venice-Mabepari wa Venisi (1969) na Julius Ceasar – Juliasi Kasari vilivyotafsiriwa na Mwl. Julius Kambarage Nyerere. Kazi hizi ni msingi wa tafsiri kwani kwa muda mrefu zimetumika katika vitabu vya kiada katika shule za upili na hata vyuo vya ualimu na vyuo vikuu. Aidha, kazi mbili za mwisho, yaani Merchants of Venice-Mabepari wa Venisi (1969) na Julius Ceasar – Juliasi Kasari siyo tu zilikuwa zimeandikwa katika Kiingereza na kufasiliwa katika Kiswahili, lakini pia aliyefanya kazi ya kuzitafsiri ni mtu aliyekuwa na ushawishi mkubwa katika maendeleo na ukuzaji wa Kiswahili nchini Tanzania. Hivyo, na watafiti waliokuwa wakichukua mwelekeo wa tafsiri, walizingatia zaidi matini zilizoandikwa katika lugha za kigeni na kuzihawilisha katika Kiswahili. Kwa mfano, Maro (2018) na Msigwa na Maro (2022) walichunguzadosari za tafsiri katika Mabango yaliyopo kwenye Barabara ya Moshi-Arusha yaliyotafsiri kutoka Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili.

Kwa kutumia njia ya uchanganuzi matini, upigaji picha; data zilikusanywa. Matokeo ya utafiti wao yalionesha kwamba, upo upotoshaji wa ujumbe na maana ya matini lengwa kutokana na wafasiri kuelekea kuhawilisha miundo ya Kiingereza katika Kiswahili. Vilevile, upotoshaji huo ulisababishwa na tofauti za kiutamaduni kati ya lugha chanzi na lengwa. Hitimisho hilo lilitolewa kutokana na kuwa lugha chanzi ni lugha ya kigeni (Kiingereza) na lugha lengwa ni Kiswahili. Hivyo, upo uwezekano mkubwa wa wafasiri kutokuwa wamilisi kikamilifu wa miundo ya lugha chanzi, yaani Kiingereza. Jambo tunalojifunza hapa ni kuwa, wafasiri wakiwa na umilisi wa lugha chanzi, uvulivuli wa tafsiri usingelitokea. Swali ambalo makala haya yanajiuliza ni kuwa, je ni wakati wote mfasiri anapokuwa mmilisi wa lugha chanzi, uvulivuli wa tafsiri unakosekana?

Mwansoko na wenzake (2015:50) wanaeleza tofauti za kiisimu zinazojitokeza katika kutafsiri Kiswahili kwenda Kiingereza na jinsi zinavyochangia kuwapo kwa dosari au uvulivuli katika lugha lengwa. Wanabainisha mfano wa matini; wasiojiweza (disabled/sio wote 'wasiojiweza' ni "disable" yaani walemavu. Kimbiza mgonjwa hospitalini (rush a patient to the hospital- mpeleke mgonjwa kwa haraka hospitalini, na sio umfukuze mbio toka huko). Wanafafanua sababu za tofauti hizi za kifasiri kuwa ni kutokana na tofauti za kiisimu kati ya lugha chanzi (Kiswahili) na lugha lengwa (Kiingereza). Hoja tunayoipata hapa ni kuwa ikiwa lugha zina mnasaba wa kiisimu haitarajiwi kupatwa na changamoto tafsiri ya matini kutokea. Swali tulilojiuliza na kujibu katika Makala haya ni kuwa, ikiwa lugha zina mnasaba mmoja wa kiisimu, ni kweli kwamba tafsiri haitakuwa na uvulivuli? Kama inavyoonekana katika mjadala huu, mifano ya lugha za tafsiri iliyohusishwa ni lugha ya kigeni na lugha ya Kiswahili. Jitihada kidogo imefanyika kuhusu tafsiri kutoka lugha asili kwenda katika lugha ya Kiswahili.

## 3.0 **Tatizo la Utafiti**

Tafiti nyingi zinazohusu uvulivuli wa matini za tafsiri umehusisha zaidi lugha ya kigeni na lugha ya Kiswahili, kama Maro (2018) na Msigwa na Maro (2022). Hitimisho linalojengwa kuhusu chanzo cha utenge huo ni kuwa zinatokana na tofauti za kiutamaduni, kiisimu na ukosefu wa umilisi wa wafasiri kwa lugha zote mbili. Kadiri ya ufahamu wetu ni tafiti chache ama hazimo kabisa zimeshughulika na uvulivuli wa matini za tafsiri kutoka lugha za asili kwenda Kiswahili. Kutofanyika kwa utafiti kama huu, mbali na mambo mengine kumesababisha kuendelea kujengeka kwa imani kwamba uvulivuli wa tafsiri unatokana na tofauti za kiisimu na kiutamaduni kati ya lugha chanzi na lugha lengwa pamoja na kutokuwa na umilisi miongoni mwa fasili kuhusu lugha wanazozitumia. Jambo ambalo tunaona linasailika kabisa. Hivyo, utafiti huu unalenga kuonesha upande mwingine wa sarafu kuhusu uvulivuli wa tafsiri na chanzo chake ukiegemea kuchanganua uvulivuli wa tafsiri ya nyimbo za Kikinga kwenda Kiswahili.

## 4.0 **Lengo la Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza uvulivuli wa matini ya tafsiri unaojitokeza kutokana na tafsiri za lugha asili kwenda lugha ya Kiswahili. Katika kutimiza hili, nyimbo tano za lugha ya Kikinga zilizoimbwa kwa lugha ya Kikinga na kutafsiriwa kwenda Kiswahili zilishughulikiwa. Kupitia uelewa wa lugha ya Kikinga, mtafiti alisikiliza matamshi ya mwimbaji na kuhusisha ujumbe uliokusudiwa katika wimbo wote. Kisha, mtafiti alilinganisha kinachosemwa na mwimbaji na maandishi yanayopeperushwa chini uso wa runinga yakifasiri maneno ya tafsiri kutoka Kikinga kwenda Kiswahili. Aina mbalimbali za tafsiri tenge zilibainishwa.

## 5.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima ilivyoasisiwa na Nida (1964) na kuendelezwa na Nida na Taber (1969). Wengine walioendeleza nadharia hii ni pamoja na Newmark (1982) na Koller (1990). Nadharia hii inashikilia kuwa usawe wa kidhima ni muhimu zaidi kuliko usawe wa kimuundo. Kwa maana kwamba, dhima ya visawe katika lugha ni muhimu kuliko kufanana kwa muundo kati ya matini chanzi na matini lengwa. Gao, (2023) akifafanunua nadharia hii anabainisha kwamba Nida (1964) alipendekeza hatua kuu nne katika mchakato wa tafsiri ambazo ni:

a) Uchanganuzi. Hatua hii ni muhimu kabisa katika mchakato wa tafsiri kwani hulenga kutafuta maana ya visawe vya matini lengwa kwa kuhusishwa na maana za matini chanzi. Kwa hivyo, umakini unahitajika kwa mfasili katika hatua hii ili kupata tafsiri iliyobora.
b) Ubadilishaji lugha. Hatua hii inahusisha kuhawilisha maana iliyopatikana kutokana na uchanganuzi wa matini chanzi kwenda matini lengwa. Ni uwekaji wa visawe vya matini lengwa badala ya vile vya matini chanzi. Yaani kuondoa maneno ya lugha chanzi na kuweka badala yake maneno ya lugha
c) Upangiliaji wa matini iliyotafsiriwa kulingana na kanuni za lugha lengwa, na
d) Ukaguzi. Hii ni hatua ya mwisho katika mchakato wa tafsiri ambapo mfasili hukagua matini lengwa ili kuona kwamba kanuni za lugha lengwa zimezingatiwa, maana hazijadoshwa au kupotoshwa.

Kwa mujibu wa nadharia hii, wafasiri wanapotafsiri kazi zao wanapaswa kuhakikisha kuwa dhima ya matini chanzi pamoja na athari zake zinajitokeza katika matini lengwa (Gao, 2023). Yaani kama matini chanzi ilikuwa inaibua hisia za kuliza hadhira kwenye matini chanzi basi na matini lengwa itimize hali hiyo hiyo. Aidha, matini chanzi ikiwa ni kufasiriwa kwa ajili ya watoto basi inatarajiwa kuandikwa kuakisi umri na uelewa wa hadhiri hiyo ambayo ni watoto. Pia, Nadharia ya Usawe wa

Kidhima inashikilia kuwa kila aina ya matini ifasiriwe kwa kuzingatia aina yake ya matini. Kwa mfano, matini za nyimbo katika Albamu ya Sumasesu Theatre Art ifasiriwe kwa kuzingatia aina hiyo ya matini na hadhira iliyokusudiwa ambayo ni jamii isiyojua lugha ya Kikinga ila Kiswahili. Yaani kazi itakayotokea inatarajiwa ifanane na matini chanzi, kama matini chanzi ni ya kisheria itakapotafsiriwa matini lengwa nayo iwe ni ya kisheria au kama matini chanzi ni ya kifasihi basi itakapotafsiriwa, matini lengwa ifanane na matini ya kifasihi. Ufanano huo utazingatia zaidi katika uteuzi wa visawe ambavyo vitafumbata dhana muhimu za kisanaa au kisheria kutegemea aina ya matini chanzi inayoshughulikiwa. Hii ina maana kwamba ujumbe ambao wasikilizaji wa matini ya kwanza waliupata ndio huo huo unatarajiwa hadhira ya matini lengwa iupate. Nadharia ya Usawe wa Kidhima inachukulia tafsiri kuwa ni mchakato wa kuwasilisha Matini lengwa (ML) kwa njia ya kutumia maneno mnasaba yasiyopotosha maaana (kuvulivulineza mnasaba)[95] baina yake na matini chanzi. Mnasaba huu hupatikana kwa njia ya usawe ambao umekitwa katika sifa majumui za lugha na utamaduni (Ghanooni, 2012). Kwamba mfasiri akabiliwapo na jukumu la kufanya tafsiri shurti atafute visawe ambavyo vinaelekea kuwa na athari sawasawa au vinakaribia kama athari alizopata msomaji wa Matini Chanzi (MC).

Nida (1964) anaainisha usawe wa aina mbili ambao mfasiri hana budi kuuzingatia ili aweze kufanya kazi yake barabara. Kwanza ni usawe wa kiumbo na pili ni usawe badilifu. Usawe wa kiumbo, ni ule unaotilia mkazo zaidi suala la umbo la matini na maudhui yabebwayo na umbo hilo kwa maana ya ujumbe katika lugha lengwa. Hii ina maana kuwa ujumbe na maumbo ya lugha lengwa vinatakiwa vioane kwa karibu kadiri inavyowezekana na vipashio mbalimbali vya lugha chanzi. Aidha, wakati usawe badilifu ni aina ya usawe wa matini lengwa (ML) kwa matini chanzi (MC) unaobadilika kwa kuzingatia zaidi athari ya kimawasiliano (Nord, 2010). Jambo la kuzingatia hapa ni namna hadhira ya ML anavyotakiwa kupata ujumbe unaoeleweka sawa na hadhira ya MC.

[95] Katika tafsiri na ukalimani upatanifu uliopo baina ya visawe/maneno au miundo iliyo na uhusiano wa kiasili, kimaana ingawa maumbo au miundo hiyo inaweza kuwa nasura au maumbo yasiyofanana katika umbo lake la nje. Ni upatanifu baina ya matini chanzi na matini lengwa kutegemea uteuzi sahihi wa visawe kutegemea athari zibebwazo na visawe hivyo kwa wasomaji wa matini lengwa.

Nida (1964) anaeleza kuwa usawe huu kuwa umekitwa katika kanuni ya athari sawa, ambapo kimsingi uhusiano baina ya wapokeaji na ujumbe unapaswa kuwa sawa kama ilivyokuwa baina ya wapokeaji na ujumbe asilia. Hii inamaana kwamba athari ya kimawasiliano ya ujumbe wa ML kwa hadhira haina budi kuwa ileile kama ilivyokuwa athari ya kimawasiliano ya ujumbe wa ML kwa hadhira chanzi. Hata hivyo, licha ya maelezo hayo ya Nida (keshatajwa) ni muhimu kutambua kuwa ni vigumu kuwa na usawe kuntu, na hivyo pengine ni vigumu kuwa na athari sawa za kimawasiliano baina ya matini chanzi na matini lengwa.

Mihimili ya Nadharia ya Usawe wa Kidhima ni pamoja na:

(i) Dhima na athari za matini chanzi ijitokeze katika matini lengwa,

(ii) Lugha ya tafsiri iwe nyepesi na ya kawaida inayoeleweka na hadhira,

(iii) Uasili wa kazi inayotafsiriwa ni muhimili mwingine wa nadharia hii, na

(iv) Uzingatiaji wa muktadha na utamaduni ambamo tafsiri inafanyika. Yaani uteuzi wa visawe vinavyotumika katika tafsiri uzingatie muktadha wa kijamii na kiutamaduni wa hadhira.

Makala haya yaliongozwa na muhimili wa (i) na (iv) unaomtaka mfasiri anapofasiri kazi yoyote azingatie muktadha na utamaduni ambamo tafsiri inafanyika kwayo. Kwa maana ya uteuzi sahihi

wa visawe vinavyobeba dhima kama ilivyokuwa katika matini chanzi. Mhimili huu unamaanisha kwamba mfasiri anapaswa kutambua maana ya maneno na kutafuta kisawe kinachofaa katika matini lengwa (ML) ili kuibua athari sawa kwa hadhira lengwa. Katika muktadha wa utafiti huu, mfasiri alikuwa akitafsiri maneno katika mazunguzo ya wimbo ambao ulikuwa unaimbwa katika lugha ya Kikinga; kisha kuweka badala yake maneno ya Kiswahili. Lengo la mfasili ilikuwa, kuwasaidia watazamaji na wasikilizaji wa nyimbo hizo ambao hawaijua lugha ya Kikinga kuelewa kile kinachoimbwa na msanii. Kwa hivyo, mfasiri, alitarajiwa kuwa na uelewa madhubuti wa visawe vya lugha ya Kiswahili ambavyo vinachukuana na vile vya lugha ya Kikinga akizingatia muktadha na utamaduni wa watumiaji wa lugha ya Kikinga. Kinyume na hapo mfasiri alikuwa analeta tafsiri iliyotenge ambayo haiendani na kile mwimbaji alichokuwa anakiwasilisha katika matini chanzi. Kwa hiyo, mhimili huu umetumiwa na makala haya ili kuweza kubainisha uvulivuli wa tafsiri kutoka Kikinga kwenda Kiswahili katika Albamu ya Sumassessu Theatre Art.

## 6.0 Uwasilishaji wa Data na Mjadala wa Matokeo

Lengo la utafiti lilikuwa ni kubainisha uvulivuli wa tafsiri zilizojidhihirisha katika matini zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kikinga kwenda lugha ya Kiswahili. Ili kufikia lengo hili, mbinu ya Uchanganuzi Matini ilitumika. Nyimbo tano kutoka kwenye Albamu ya Sumasesu Theatre Art Group zilichunguzwa. Nyimbo hizi ni kama zifuatazo na tafsiri yake katika mabano: Ikhilunga (Dunia), Kihumile kukyanya (Kimetoka Juu), Vilila aAana (Wanalia watoto), Ndisaga (Ninawaza) na Vakinga (Wakinga). Mtafiti alisikiliza nyimbo hizo mara tatu huku akilinganisha maneno au miundo iliyokuwa inaimbwa na msanii na tafsiri iliyofanywa kupitia maandishi yaliyopitishwa chini yake kufasili maana za maneno. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima ya Nida(1964) katika muhimili wa uzingatiaji wa muktadha na utamaduni na athari sawa kwa hadhira mtafiti aliweza kutathimini tafsiri iliyotolewa na hivyo; alibaini makossa mbalimbali kama

### Jedwali Na. 1.1: Tafsiri tenge kutoka Kikinga kwenda Kiswahili

| Na. | MC | MLU | MLS | Wimbo |
|---|---|---|---|---|
| i. | Avamama vasambwikhe | …akina mama wamechanganyikwa… badala ya akina mama ***wamebadilika***… | …akina wamegeuka (wamebadilika)… | **Ndisaga** (Ninawaza) |
| ii. | Üvöbanga | … uongo… badala ya … ***utundu***… | … utundu | |
| iii. | …Vanyakiosa kölëkëki kö Mbeya? | Wanyakyusa hali ikoje Mbeya? Badala ya ***kuna nini*** Mbeya? | … Wanyakyusa kuna nini Mbeya? | **Vakinga** (Wakinga) |
| iv. | …Vabena kölëkëki kö Nsombe? | …Wabena hali ikoje Njombe badala ya ***kuna nini*** Njombe? | … Webena kuna nini Njombe? | |
| v. | … Vahehe kölëkëki kwî Linga? | …Wahehe hali ikoje Iringa? Badala ya ***kuna nini*** Iringa? | … Wahehe kuna nini Iringa? | **Vilila Ana** (Wanalia watoto) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| vi. | …Valugulu kölĕkiki kö Mologolo? | … Waluguru ***hali ikoje***… badala ya ***kuna nini***… Morogoro? | … Waluguru kuna nini Morogoro? | |
| vii. | … Mtawa kölĕkĕki kwî Konda? | … Mtawa hali ***ikoje*** Ikonda? Badala ya … ***kuna nini*** Ikonda? | … Mtawa kuna nini Ikonda? | |
| viii. | … *lönga (lönganitse)… | …***unga...*** badala ya …unganisha… | …alichounganisha… | |
| ix. | …kyakyula… (*Siinu*) | …chakula… bdala ya … ***vitu***… | | **Ikhilunga** |
| x. | … sianzo…(*löhömu*) | … vyanzo… | | |
| xi. | … kyakyotosa… (*siolosu*)... | … chakutosha… | …kingi… | |
| xii. | … migunda… (silemela) | … mashamba… | …migunda… | |
| xiii. | …lweli… (*siitso*) | …kweli… | … sana… | **Kihumile Kukyanya** (Kimetoka Juu) |

**Chanzo:** Data za Utafiti, 2023

**Ufunguo:**
**MC** Matini Chanzi
**MLU** Matini Lengwa yenye uvulivuli/dosari
**MLS** Matini Lengwa Sahihi

Katika jedwali la 1.1 MC ni matini chanzi; ML ni matini lengwa ambayo ina dosari za kitafsiri na MLS ni matini lengwa sahihi. Kama data za utafiti zinavyoonesha katika jedwali 1.1 hapo juu; kuna uvulivuli katika tafsiri iliyofanyika kupitia matini za nyimbo za lugha ya Kikinga kwenda katika lugha ya Kiswahili. Sehemu inayofuata inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti yaliyobainishwa katika jedwali na. 1.1 hapo juu.

## 6.1 Uvulivuli wa Tafsiri kutokana na Mbinu ya Tafsiri

Data katika jedwali 1.1 hapo juu kwenye mfano wa kwanza inaonesha uvulivuli wa tafsiri. Matini ya chanzi ni (…. avamama vasambwikhe) kwa maana ya wanawake wamebadilika au wameharibika na kutafsiriwa kuwa (… akina mama wamechanganyikwa). Katika tafsiri hii mambo mawili yanajitokeza na kuleta uvulivuli wa tafsiri hii. Kwanza ni mbinu iliyotumika kutafsiri ambayo ni mbinu ya tafsiri sisisi (ava mama na kutafsiriwa akina mama). Hii ni mbinu ya tafsiri sisisi. Tafsiri sisisi ni miongoni mwa mbinu itumikayo kufanya tafsiri lakini, siyo nzuri kwa matini zinazolenga mawasiliano bali lazima itumike kwa pamoja na tafsiri nyinginezo kuwasilisha ujumbe wa kimawasiliano. Wanjala (2016:70) anasema "tafsiriri sisisi aghalabu hutoa tafsiri potofu na kwa hivyo, huwa na uwezekano wa kuleta utata na hasara katika mawasiliano". Mfasiri katika matini hii ametumia tafsiri sisisi kusababisha uteuzi usiosahihi wa visawe mwafaka vya kujenga mawasiliano sahihi. Hali hii inakinzana na mawazo ya Nida na Tiber (1969) kama yaliyobainishwa vizuri na Gao (2023) kuwa tafsiri sio tu sanaa lakini pia ni mawasiliano. Utumizi wa tafsiri sisisi

unafanya mawasiliano yasiweze kufanyika kwa ufasaha kama ilivyokusudiwa na msanii.

Kadhalika, uteuzi usio sahihi wa visawe katika matini lengwa. Matini chanzi inasema avamama vasambwikhe kwa maana ya wanawake wamebadilika; lakini mfasiri ametafsiri kama (…akina mama wamechanganyikiwa…). Kuchanganyikiwa ni hali ya mtu kurukwa na akili. Uteuzi wa kisawe cha akina mama wamechanganyikiwa unaelekea kupotosha kabisa maana ya msingi iliyokusudiwa na msanii. Kama asemavyo Gao (2023), mingoni mwa dhima ya tafsiri ni kuwafanya wasomaji (watazamaji)wayaelewa matini chanzi. Matumizi ya kisawe wamechanganyikiwa, kinafanya wasomaji au wasikilizaji kutoyaelewa kabisa matini chanzi. TUKI (2019:68), wanafafanua kuchanganyikiwa kwamba ni kuwa katika hali ya kubabaika au kukosa utulivu; wakati Oxford (2016:55) wanafasili kuchanganyikiwa kuwa kutokuwa na utulivu wa akili na kufanya mambo yasiyoeleweka; kuwa na kichaa. Kadhalika, JKF (2016:64) wanafasilikuchanganyikiwa kuwa ni (ku)pungukiwa na akili. Fasili zote hizi zinaonesha kuchanganyikiwa nikupoteza akili na kuwa katika hali ya kutojitambua. Hata hivyo, MC haioneshi ikiwa wanawake wanafanya matendo wafanyayo kutokana na kurukwa na akili, bali hufanya matendo hayo wakiwana akili zao timamu. Kwa hiyo, kulingana na matini chanzi, avamama vasambwikhe inarejelea wanawake ambao ni watu wazima waliobadili tabia na kuanza kujihusisha na masuala ya kingonona wavulana wadogo ambao ni sawa na watoto wa kuwazaa. Siyo kwamba ni vichaa kamamfasiri anavyoelekeza kwenye tafsiri yake. Matumizi ya kisawe wamechanganyikiwa katika tafsirikama ilivyotumiwa na mfasiri katika wimbo wa Ndisaga (Ninawaza) si sahihi. Muhimili wa Nadharia ya Usawe wa Kidhima unaomtaka mfasiri kuteua visawe ambavyo vinazingatia muktadhana utamaduni. Katika fasili hii, muktadha na utamaduni wa lugha chanizi vyote havikuzingatiwa. Kadhalika, hitajio la kinadharia ya usawe wa kidhima linalotaka athari alizozipata hadhira wa matini chanzi ndizo hizo azipate hadhiri wa matini lengwa haliekei kufikiwa, kwani maana ya msingi itokayanayo na tafsiri hiyo imepotea.

Mfasiri ametumia viulizi vinavyotumiwa na nomino zinazoangukia ngeli ya [i-zi]. Kwa hivyo, matumizi ya kisawe hali ikoje, siyo sahihi kwa sababu kiulizi katika matini chanzi kipo katika ngeli [i-zi] na hapa mfasiri amepeleka katika ngeli [pa-mu-ku]. Hali hii ni tofauti na msingi wa Nadharia ya Usawe wa Kidhima unaohitaji kuwa, aina ya matini itafsiriwe kwa kuzingatia aina hiyo ya matini ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa mofolojia ya maneno kutoka matini chanzi. Kilichofanywa na mfasiri kinakwenda kinyume na mtazamo wa Gao (2023) na Zhao na wenzake (2019), wanapozunguzumzia uzingativu wa sarufi ya lugha lengwa katika tafsiri. Tafsiri ambayo Hivyo, tafsiri hiyo ni tenge kwa kuzingatia mhimili wa Nadharia ya Usawe Kidhima unaosisitiza kuwa, uteuzi wa visawe katika tafsiri uzingatie muktadha na utamaduni ambamo tafsiri inafanyika. Yaani uteuzi wa visawe vinavyotumika katika tafsiri uzingatie muktadha wa kijamii na kiutamaduni wa hadhira

## 6.2 Uvulivuli wa tafsiri kutokana na Kupotosha Maana

Data kutoka katika jedwali 1.1 hapo juu kwenye mfano wa (ii) inaonesha uvulivuli wa tafsiri ambayo imesababishwa na kupotosha maana. Matini chanzi (üvöbanga) ikiwa na maana ya uongo katika lugha ya Kiswahili na kufasiriwa kama utundu. Matini imedondolewa kutoka katika wimbo wa kwanza katika Albamu. Kwa ujumla wimbo huu unahusu watoto wa shule za sekondari wanavyowadanganya wazazi au walezi wao kwamba wanakwenda shuleni kumbe wanakwenda katika majumba ya starehe (nyumba za kulala wageni (gesti) na wanaume ili kufanya ngono). Wahusika waliooneshwa katika wimbo huo, ni wasichana wakiwadanganya wazazi ama walezi wao asubuhi na kupewa nauli lakini wanaishia katika nyumba za kulala wageni bila kwenda shuleni; na

jioni wanarejea nyumbani kama kwamba wametoka shuleni. Uteuzi wa kisawe utundu kama tafsiri ya neno üvöbanga siyo sahihi kwa kuzingatia muktadha wa wimbo na ujumbe unaorejelewa. Katika MC, watoto hasa wakike wanawadanganya wazazi/walezi kuwa wanakwenda shuleni ilihali hawaendi na kuishia kufanya masuala ya ngono na watu wenye pesa. Watoto hawa wanasema uongo kwa wazazi na walezi wao. Video za wimbo huo zinaonesha wanafunzi wakipanda magari makubwa ya wanaume aina ya Prado na kuingia nyumba za kulala wageni wakiwa na sare za shule wakati wazazi au walezi wao wakijua watoto wamekwenda shuleni kusoma. Zaidi ya hayo, wanaporudi jioni, watoto hawa wanasema uongo wa kueleza mahitaji yaliyoagizwa na walimu shuleni wakati hayo maagizo hayakutolewa na wala watoto wenyewe hawakwenda shuleni. Tafsiri iliyotumika haimpi hadhira wa matini lengwa athari sawa na athari aliyopata hadhira wa matini chanzi. Mfasiri anaelekea alizingatia jambo moja la matendo yafanywayo na watoto hawa na kusahau kabisa mawasiliano yaliyokuwa yanafanyika na wahusika ama na wazazi wao au na wale wanaoume ambao ndiyo kusudio kiini la wimbo. Kutozingatia mawasiliano, kunakwenda kinyume na Nadharia ya Usawe wa Kidhima kama inavyoshadidiwa na Weibin (2019), kwamba uchaguzi wa visawe katika tafsiri uzingatie suala la mawasiliano. Jambo hili, linakwenda kinyume na mhimili wa Nadharia ya Usawe wa Kidhima usemao, hadhiri wa matini lengwa anastahili apate athari sawia ya ujumbe kama alivyopata hadhira wa matini chanzi.

## 6.3 Uvulivuli wa Tafsiri kutokana na Kubadilisha Visawe vya Ngeli

Kama jedwali 1.1 linavyoonesha kuna uvulivuli utokanao na mfasiri kuteua visawe vya ngeli tofauti kutoka matini chanzi kwenda matini lengwa. Massamba (2016) anaeleza kwamba, ngeli ni utaratibu wa uainishaji makundi ya maneno au vipashio vyenye sifa zinazofanana. Katika jedwali 1.1 hapo juu mfano wa (iii) unaonesha matini chanzi (…Vanyakiösa kölĕkĕki kö Mbeya?) na kutafsiriwa kama (Wanyakyusa hali ikoje Mbeya?).

Matini hii imedondolewa kutoka kwenye wimbo wa Vakinga (Wakinga). Ujumbe wa wimbo huu uko katika mfumo wa maswali, ambapo msanii anauliza hali mbalimbali zilivyo katika jamii husiani. Ametaja jamii anuwai kama vile, Wabena, Waluguru na Wahehe kwa uchache. Hata hivyo,kiulizi (kölĕkĕki kö) ina maana ya (kuna nini huko?). Katika mwainisho wa ngeli, kiulizi hiki kinahusiana na nomino za ngeli ya [pa-mu-ku]. ingekuwa ni mwafaka hapa ilipaswa kuwa ni (…Wanyakyusa kuna nini Mbeya?). Swali kuna nini Mbeya? Na hali ikoje Mbeya? Kimaana siyo sawa. Kwa hiyo, hadhira ya matini lengwa haikupata athari sawa kama walizopata hadhira ya matinichanzi. Jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Nadharia ya Usawe wa Kidhima ya athari sawa kwa wote. Aidha, uchunguzi zaidi unaonesha kuwa mfasiri anatatizo la kutojua mofu //-kö-// katikalugha ya Kikinga ina maana gani, kwa sababu kila ilipotumika mofu hiyo, katika kufasiri alifanya makosa ya kitafsiri kwa kushindwa kuteua kisawe kamili. Kushindwa huko kujua maana ya mofu //-kö-//, kumefanya kushindwa kuteu kwa usahihi visawe vya lugha ya Kiswahili na hata kusababisha maana ya MC kupotoshwa. Mathalni msanii anauliza Wabena kuna nini huko Njombe; lakini mfasili anasema hali ikoje huko Njombe. Kiulizi kuna nini na ikoje vina maana tofauti kabisa na huangukia katika ngeli tofauti kama tuliyoonesha hapo juu. Mifano zaidi ni kama inavyoonesh-wa katika jedwali 1.2.

## Jedwali Na. 1.2: Uvulivuli wa Tafsiri kutokana na Mabadiliko ya ngeli

| Na. | MC | MLU | MLS |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| si. | …Vabena kölĕkĕki kö Nsombe? | …Wabena hali ikoje Njombe | … Webena kuna nini Njombe? |
| ii. | … Vahehe kölĕkĕki kwî Linga? | …Wahehe hali ikoje Iringa? | … Wahehe kuna nini Iringa? |
| iii. | …Valugulu kölĕkiki kö Mologolo? | … Waluguru hali ikoje Morogoro? | … Waluguru kuna nini Morogoro? |
| iv. | … Mtawa kölĕkĕki kwî Konda? | … Mtawa hali ikoje Ikonda? | … Mtawa kuna nini Ikonda? |

**Chanzo:** Data za Utafiti, 2023

Data katika jedwali la hapo juu zinaonesha mfasiri kushindwa kuteua mofu sahihi kwa kuzingatia ngeli za maneno katika lugha ya Kiswahili.

## 6.4 Uvulivuli wa tafsiri kutokana na Makosa ya Matini chanzi

Data katika jedwali na. 1.1 hapo juu kutoka kwenye mfano wa (viii) inaonesha matini chanzi kuwa na kasoro. Katika matini chanzi, kitenzi *lönga (unga) kimekosewa badala ya kuwa … lönganitse… kwa maana ya unganisha. Matini chanzi imechukua maelezo yake kutoka katika maandiko matakatifu yanayohusu ndoa za kikristo. Katika maandiko hayo kasisi au mchungaji hutamka maneno fulani anapofungisha ndoa au anapowaapisha wafunga ndoa. Kiapo hiki kipo katika hali ya kutendesha (unganisha) lakini matini chanzi ipo katika hali ya kutenda lönga (unga). Kiapo hiki husomeka kuwa, alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe. Kile kilichokuwa kinaimbwa kinatofautiana na kile kilichotafsiriwa katika maandishi yanayopita katika uso wa runinga. Hivyo, fasiri ya kitenzi lönga kuwa unganisha siyo sawa kwa kuzingatia Nadharia ya Usawe wa Kidhima.

Kimofolojia, neno linaponyambulishwa katika hali ya kutendesha hupanua maana yake tofauti na linapokuwa katika hali ya kutenda. Aidha, ni Imani yetu kuwa kwa tafsiri hii hadhira wa Matini Lengwa anapata athari tofuati na ile ambayo hadhira wa matini chanzi aliipata. Matokeo haya yanaendana na mhimili wa kwanza wa nadharia unaosema dhima na athari za matini chanzi ijitokeze katika matini lengwa.

Vilevile, mfano mwingine wa tafsiri tenge kutokana na matini chanzi ni yale yanayomfanya mfasiri kuteua kimakosa kisawe cha matini lengwa …kyakyula… (siinu) na kutafsiriwa kama …chakula… Kuteua moja kwa moja kisawe cha …kyakyula… kuwa ni chakula katika muktadha wa wimbo Ikhilunga kwa maana ya Dunia haikuwa sahihi. Katika wimbo huo, sinu uliashiria vitu mbalimbali na siyo chakula pekee. Kwamba, utunzaji wa mazingira na vilivyomo ukifanyika vema ikiwa ni pamoja na kujieupusha kuendesha shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji ndiko kutakakoleta vitu mbalimbali vya kutosha ikiwamo maji, mvua, chakula nakadhalika, wala siyo chakula pekee kama mfasiri alivyofanya. Kisawe sahihi katika matini chanzi kilitarajiwa kuwa ni siinu yaani vitu mbalimbali. Uteuzi wa kisawe hicho chakula kumeifinya maana iliyokusudiwa na msanii. Kama tulivyodokeza hapo juu, katika lugha ya Kikinga siini ni vitu na siyo chakula pekee. Hivyo, hoja ya Nadharia ya Usawe wa Kidhima katika muhimili wake unaohitaji athari alizopata hadhira ya matini chanzi kujitokeza kwa hadhiria wa matini lengwa haujazingatiwa na fasiri hii. Kwasababu, hadhira wa matini chanzi alipata maana zaidi kuliko hadhira wa matini lengwa.
Mifano zaidi mingine ya tafsiri tenge kutokana na makosa ya matini chanzi ni kama

yanavyobainsshwa katika Jedwali 1.3 hapa chini:

**Jedwali Na. 1.3: Uvulivuli wa tafsiri kutokana na Makosa yaliyomo katika matini chanzi**

| Na. | MC | ML | MLS |
|---|---|---|---|
| i. | *… sianzo…(*löhömu*) | … vyanzo… | …vyanzo… |
| ii. | … kyakyotosa… (*siolosu*)... | … chakutosha… | …kingi… |
| iii. | … migunda… (silemela) | … mashamba… | …migunda… |
| iv. | …lweli… (*siitso*) | …kweli… | … sana… |

**Chanzo:** Data za Utafiti, 2023.

Data katika jedwali Na. 1.3 zinaonesha uvulivuli wa tafsiri kutokana na makosa yaliyomo katika matini chanzi kiasi kwamba mfasiri alipojaribu kuteua visawe vya matini lengwa ama alipopunguza maana iliyokusudiwa na msanii, au alipanua mawanda ya maana hiyo. Hali hiyo imeenda kinyume na Nadharia ya Usawe wa Kidhima katika muhimili wa (iv) hapo juu unaosema; uzingatiaji wa muktadha na utamaduni ambamo tafsiri inafanyika. Yaani uteuzi wa visawe vinavyotumika katika tafsiri uzingatie muktadha wa kijamii na kiutamaduni wa hadhira.

## 7.0 Hitimisho

Makala haya yalilenga kuchunguza uvulivuli wa tafasiri kutoka Kikinga kwenda Kiswahili katika matini ya nyimbo zilizomo katika Albamu ya Sumasesu Theatre Art Group. Msingi wa uchunguzi huu, ulitokana na madhanio ya tafiti nyingi tangulizi kuhusu utenge wa tafsiri; kwamba zinatokana uelewa mdogo wa kiisimu wa lugha miongoni mwa wafasili. Tafiti chache sana, zimejishughulisha na utenge wa tafsiri kutoka lugha asilia kwenda katika lugha ya Kiswahili. Chanzo cha data za utafiti huu ni Maktabani. Sampuli ya nyimbo tano zilihusishwa kama sampuli ya utafiti, zilizopatikana kwa njia ya usampulishaji tabakishi. Katika uchanganuzi wa data, nyimbo zilisikilizwa mara tatu huku uchunguzi wa maandishi yaliyokuwa yanapita katika uso wa runinga yalikuwa yakitathiminiwa. Maandisho hayo, ni tafsiri ya Kikinga kwenda lugha ya Kiswahili. Kwakuongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima (Nida, 1964) kama ilivyoendelezwa na Nida na Taber (1969) ilizingatiwa. Utafiti umebaini uvulivuli wa tafsiri hasa uteuzi usiyo sahihi wa visawevya Kiswahili ikizingatia muktadha wa matumizi ya nyimbo zilizohusika. Uteuzi huo umesababisha ama kupotosha maana kwa kuifinya au kuipanua maana hiyo. Kadhalika katika maeneo mengine, uteuzi huu umefanya ujumbe wa awali ubadilike kabisa. Yaani hadhiria ya ML imepata athari tofauti na ile ambayo hadhira ya MC ilipata. Sababu ya huo uvulivuli wa tafsiri imetokana na mfasili kuelekea kutokuwa na umahiri wa tafsiri; yaani mfasiri anaweza kuzungumzalugha zote mbili Kiswahili na Kikinga, ila hana ujuzi wa tafsiri. Kadhalika anaelekea hana kabisa uelewa wa kiisimu wa lugha zinazohusika. Kwa mfano, anaelekea haoni tofauti ya siinu1 (vyakula) na siinu2 (vitu). Katika Kikinga neno siinu ni homonimu. Mfasili anaelekea hana ufahamu huo. Aidha, imeonekana pia kwamba kuna sehemu nyingine uvulivuli wa tafsiri hiyo umechangiwa na kasoro za matini chanzi, hivyo, kutatiza tafsiri iliyotolewa. Katika kukosewa kwa MC imeonekana uteuzi wa visawe vya tafsiri kuachana na matini kwa ama kufinya maana iliyokusudiwa au kupanua maana. Makala

yanapendekeza kuwa utafiti mwingine wa kina zaidi ufanyike katika kuchunguza uvulivuli wa tafsiri kutoka lugha za asili kwenda Kiswahili ili kupanua data na hivyo, kuwa na uwezekano wa kutolewa kwa mahitimisho ambayo yataongeza maarifa ya kinadharia kuhusu uvulivuli wa tafsiri.

## Marejeleo

Cartford, J. C. (1995). A Linguistic Theory of Translation. London: Heinmann.
Chen, W. (2019). Approaches to Contradictions of Translation. Peking: Peking University Press.
Gao, Y. (2023). Analysis of Eugene Nida's Translation Theory. Katika International Journal of Education and Humanities. Juzu. 10, Na. 1.
Ghanooni, A. R. (2012). A Review of the History of Translation Studies: Theory and Practice in Language Studies. (Toleo la 2). Ufini: Academy Publisher.
JKF, (2016). Kamusi Elezi ya Kiswahili. The Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.
Koller, W. (1990). The Concept of Equivalent and the Object of Translation Studies. Norway: University of Bergen Publisher.
Maro, J. R. (2018). Dosari za Tafsiri katika Mabango kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.
Massamba, D. P. B. (2016). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. TUKI: Dar es Salaam.
Msigwa, A. B. G. na Maro, J. R. (2022). Uvulivuli wa Tafsiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili katika Mabango yaliyopo Barabara Kuu ya Moshi-Arusha. Katika Jarida la CHALUFAKITA. Juz. (4), uk. 15-30. TUKI: Dar es Salaam.
Mwansoko, H. J. M., Mekacha, R. D. K., Masoko, D. L. W., na Mtesigwa, P. C. K. (2015), Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu. Dar es Salaam: TUKI.
Newmark, P. (1982). Approaches to Translation. Oxford na New York: Pergamon Press.
Nida, E. A. (1964). Towards a Science of Translation. Leiden: E. J. Brill.
Nida, E. A. na Taber, C. R. (1969). The Theory and Practice of Translation. London: Prentice Hall.
Nord, C. (2010). "Functionalist Approaches" katika Gambier, Y na Van Doorslaer, L. Handbook of Translation Studies. Amsterdam/ Philadelphia: John Benjamins Publishing Company. Juz 1. Uk 120-128.
Oxford, (2016). Kamusi Sanifu ya Msingi. Oxford University Press: Nairobi.
TUKI, (2019). Kamusi ya Kiswahili Sanifu (toleo la 4). Oxford University Press: Nairobi.
Wanjala, S. (2016). Misingi ya Ukalimani na Tafsiri: Kwa Shule, Vyuo na Ndaki. Serengeti Bookshop: Mwanza.
Zhao, J. Zurui, He, na Jing, Du (2019). An Analysis of Nida and Newmark's Translation Theory. Katika Overseas English. Juzu. (06).